TAARIFA YA MKURUGENZI MTENDAJI KWA BARAZA LA MADIWANI

Mhe. Mgeni Rasmi, Mkuu wa Wilaya ya Muleba
Mhe. Mwenyekiti wa Halmashauri (W)
Mhe Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri (W)
Waheshimiwa Madiwani
Ndugu Wataalam
Ndugu Wananchi
Mabibi na Mabwana

UTANGULIZI

Leo tena tunafurahi kufanya kikao chetu cha Baraza la Madiwani katika wilaya yetu, kikao hiki kikiwa ni cha mwisho wa mwaka wa fedha 2016/2017. Tunamshukuru Mungu ambaye kwa rehema zake ametujalia nguvu na afya hata tukaweza kufanya yale yaliyowezekana. Tumetekeleza mengi, na kuona mafanikio ya uongozi wenu (Waheshimiwa madiwani) na utayari wa watendaji. Jambo la umoja huu, limetufanya tupate mafanikio mengi na kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi wetu.

MAMBO MAKUU YALIYOTOKEA

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, tumeshuhudia mambo makubwa kadhaa mengine yakiwa mazuri na mengine yakituumiza. Tumeshuhudia tetemeko la ardhi ambalo limetusababishia uharibifu wa miundo mbinu kuanzia ngazi ya familia hadi kweye taasisi mbali mbali za kiserikali. Tumeshuhudia ukame mkali uliosababisha upungufu wa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Tumeshuhudia baadhi ya watumishi wakiachishwa kazi baada ya uhakiki mbali mbali uliofanyika kitaifa, na baadhi ya watumishi kuaga dunia; Mungu awarehemu.

Na kwa upande mwingine tumeshuhudia kuongezeka kwa watumishi wapya waliorudishwa kazini baada ya kuwa wamesimamishwa wakati wa uhakiki. Tumeshuhudia uendeshaji wa uchaguzi mdogo na kujaza nafasi wazi ya Mheshimiwa diwani wa kata ya Kimwani.

UENDESHAJI WA OFISI NA SHUGHULI ZA KAWAIDA ZA HALMASHAURI

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri yetu imeendelea kuendesha ofisi zake zote zilizosambaa katika vijiji, kata na ofisi kuu ya halmashauri. Pia tumefanikiwa kusimamia na kuendesha shughuli za kawaida za Halmashauri kwa kufanya malipo muhimu yaliyohitajika, kwa kadri ya upatikanaji wa fedha na kwa kuzingatia vipaumbele vyetu.

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri yetu ilikadiria kukusanya na kutumia jumla ya Tsh 2,517,972,259 kutoka vyanzo vyake vya ndani na kufanikiwa kukusanya jumla ya Tshs. 2,659,903,714.37 sawa na asilimia 106 na kutumia Jumla ya Tsh. 2,253,920,595.

Aidha Halmashauri ilikadiria kupokea na kutumia Jumla ya Tsh. 36,237,758,000 kutoka Serikali kuu. Hadi kufikia 30/06/2017 Halmashauri imetumia kiasi cha Tsh. 27,282,486,481.

UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UWEKEZAJI NA VIWANDA

Ili kuweka msingi imara wa uwekezaji na viwanda hapa wilayani na kuwawezesha wananchi kunufaika na maslahi mapana ya uchumi wa kati kama inavyohimiza Serikali ya Awamu ya Tano kwa mwaka 2016 /2017 Halmashauri yetu imejitahidi kuhimiza serikali za vijiji kutenga maeneo ya shughuli za uwekezaji kwa huduma za jamii , biashara na viwanda. Kutokana jitihada hizo halmashauri imepokea jumla ya maeneo 104 yaliyopendekezwa na kutengwa kutoka vijiji 83 vya kata 36 kati ya kata 39 zilizowasilisha maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vidogo vidogo na shughuli za kijamii yenye ukubwa wa takribani hektari za mraba 321.7708.

Kwa kipindi hiki Halmashauri ya Wilaya kwa kutumia wataalamu wake imekusanya takwimu za shughuli za viwanda vidogo vidogo. Imeonekana kuwa kuna wajasiriamali wanaojishughulisha na uzalishaji wa bidhaa mbali mbali wapatao 147. Wazalishaji hawa wanajishughulisha na utoaji wa huduma mbali mbali na bidhaa kwa wananchi wa wilaya hii.. Vile vile halmashauri imebaini na kupendekeza maeneo saba kuwa ya kipaumbele kwa ajili ya uwekezaji kutokana na umuhimu wake kiuchumi.

Kwa upande wa maeneo hayo muhimu ya ardhi kiuchumi kwa ajili ya shughuli za uwekezaji ya Halmashauri; uandishi wa maandiko na michoro kwa ajili ya

kuombea fedha ya ujenzi wa majengo na miundombinu maeneo mbali mbali umefanyika. Wataalam wa Idara ya Mipango wakishirikiana na wale wa Idara ya Ujenzi wa hapa wilayani waliandaa michoro na maandiko kwa ajili ya maombi ya fedha ya kugharamia utekelezaji wa miradi 3 ya maendeleo. Maandiko hayo yaliwasilishwa katika Manejimenti ya Benki ya NMB MULEBA ambayo nina uhakika yakikubaliwa yatafanikisha utekelezaji wa miradi yenye thamani ya Tshs1,342,032,310.

Halmashauri inaendelea kufanya jitihada kuhakikisha maeneo ya uwekezaji yaliyosalia uendelezaji wake unafanyika. Kwa kutilia maanani kuwa uwekezaji katika baadhi ya miradi unahitaji kiasi kikubwa cha fedha. Kwa hali hiyo uendelezaji huu unatarajiwa kufanyika kwa utumiaji wa mbinu mbali mbali zikiwemo za uhusishwaji wa sekta binafsi na utafutaji wa raslimali kutoka taasisi za kifedha za hapa ndani ya nchi kulingana na taratibu na miongozo inayotolewa na serikali.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/2017, tumefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali ambayo imechangiwa kutoka vyanzo mbali mbali, vikiwemo vya Mapato ya Ndani, Ruzuku ya maendeleo, Mfuko wa Barabara, Programu ya Maji vijijini, Mpango wa Maendeleo ya Elimu Sekondari, Program ya TASAF, “Perfomance for Result” na Miradi ya umwagiliaji. Jumla ya Tshs. 8,934,818,499.56 zimepokelewa na Tshs. 7,847,302,416.33 zimetumika katika miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa CDG fedha zilizotolewa ni Tsh. 680,008,000.00 na zimetumika kutekeleza shughuli zifatavyo;

- Ujenzi wa bwalo katika shule ya sekondali Nyailigamba
- Ujenzi wa zahanati ya Mafumbo, Kerebe na Ikuza.
- Ujenzi wa soko la ndizi la Mkaliambwa.
- Ujenzi wa mwalo wa Katembe umeboreshwa, Ghala limekarabatiwa, uchimbaji wa choo umekamilika
- deni la ukarabati wa ofisi ya mkurugenzi limelipwa
- Kulipa deni la ujenzi wa nyumba ya mtumishi muleba limelipwa
- Kufanya mafunzo ya planrep kwa wakuu wa idara, katibu muhtasi na maafisa bajeti wa idara
- Kufanya mafunzo ya uwaandaji wa mipango kwa kutumia mfumo wa fursa na vikwazo kwa waheshimiwa Madiwani.
- Kufanya usimamizi na ufatiliaji wa miradi ya maendeleo

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa program ya maji vijijini fedha zilizotolewa ni Tsh. 39,404,179.93 ndani ya bajeti na nje ya bajeti Tsh. 830,701,793.65 na zimetumika kutekeleza shughuli zifatavyo:- ujenzi wa skimu za maji katika vijiji vya Ruhanga, Kamachumu, Kangaza, Magata/Karutanga, Katembe, Kamachumu II, Kishoju na Katoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mfuko wa barabara fedha zilizotolewa ni Tsh. 576,357,432.00 ndani ya bajeti na nje ya bajetii ni Tsh. 502,971,729.79 zimetumika kutekeleza shughuli zifatavyo; kulipia madeni ya barabara ambazo tayari zimekamilika na barabara nyingine kazi zinaendelea mfano matengenezo ya muda maalum km 30.84, matengenezo sehemu korofi km 12.6, matengenezo ya kawaida Tsh. 108.9, matengenezo ya makalvati 28 na ujenzi wa madaraja 6.

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa upande wa fedha ya TASAF kiasi cha Tsh. 3,280,727,330.00 zimetumika kuwezesha kaya masikini sana 14,896 katika vijiji 109 kupata ruzuku kupitia mfuko wa TASAF.

Mheshimiwa mwenyekiti, kiasi cha Tsh. 12,866,156.00 zimetolewa kwa ajili ya Usafi na Mazingira na kutumika katika kutekeleza kampeni ya usafi wa mazingira kwa awamu ya kwanza.

Mheshimiwa mwenyekiti kiasi cha Tsh. 447,535,087.29 zimetolewa program ya maji Vijiji na zimetumika katika kutekeleza miradi ya maji vijijini. kwa shughuli zifuatazo, ujenzi wa skimu za maji katika vijiji Ruhanga, Kamachumu II, Kamachumu I, Kangaza, Magata/Karutanga, Katembe, Kishoju na Katoke.

Mheshimiwa mwenyekiti, kwa upande wa fedha ya P4R shule za msingi kiasi cha Tsh. 398,332,281.00 kimetumika katika kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- Ujenzi wa nyumba ya walimu 1(six in one) katika Shule ya Msingi Byengeragere;
- Ujenzi wa vyumba 4 vya madarasa, ofisi 1 ya walimu, na vyoo vya wanafunzi matundu 20 vimejengwa katika shule ya msingi Nyailigamba
- Ujenzi wa vyumba vya madarasa shule za msingi Kyabishagao, Kitanga, Mkombozi, Kagogo, Katoma Kahumulo, kikuku na Katanda
- Ujenzi wa matundu ya vyoo katika shule za msingi Akajunguti, Katanga, na Nyakishozi ;
- Ukamilishaji wa Vyumba vya Madarasa katika shule za msingi Manyora, Rwenshato, Igabiro, Bukambira, Iroba, Kairungu, Magata, Rulanda, Nyakabango, Murungu, Kasindaga, Kashumbililo, Makongora B , Rwazi, Lyamabumbe, Omurunazi, Magenyi, Kashenge, Buyaga na Kagondo A.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa fedha ya P4R kwa shule za sekondari kiasi cha Tsh. 783,701,740.98 kimetumika katika kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- Ujenzi wa madarasa 6, nyumba 2 za walimu, matundu 10 ya vyoo, jengo la utawala na kumalizia miundombinu iliyopo katika Shule ya Sekondari Prof. Joyce Ndalichako;
- Ujenzi wa madarasa 4, mabweni 2, matundu 10 ya vyoo pamoja na kukarabati maabara 3 katika Shule ya Sekondari ya Nyaligamba
- Ujenzi wa bweni 1, Vyumba 2 vya madarasa, kujenga matundu 10 ya vyoo na kukarabati vyumba 2 vya madarasa katika Shule ya Sekondari Ngenge
- kupandisha kuta, kupiga renta na kuezeka katika Shule ya Sekondari Mubuka
- Kuezeka chumba cha darasa Shule ya Sekondari Anna Tibaijuka;
- Ujenzi unaendelea na umefikia hatua ya kuezeka Shule ya Sekondari Mayondwe
- Kupandisha kuta ya maabara moja pamoja na kuweka msingi wa maabara ya pili Shule ya Sekondari Kishanda;
- Vyumba vinne vimeezekwa na uwekaji wa plasta katika Shule ya Sekondari Bujumba;
- Ujenzi wa matundu manne ya vyoo vya wanafunzi(Wav& Was) katika Shule ya Sekondari Biirabo;
- Kufanya umaliziaji katika kuta, paa na sakafu katika matundu ya vyoo na bafu katika Shule ya Sekondari Nyaligamba;
- Ujenzi wa kuta, kujenga paa, kupiga ripu na kujenga sakafu vyoo katika Shule ya Sekondari Kagoma;
- Kumalizia ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa katika Shule ya Sekondari Ibuga
- Kuweka miundo mbinu ya ndani (maji,umeme na gesi) ya chumba 1 cha maabara.Nyakatanga;
- Kukarabati sakafu,mbao za kufundishia,paa na kuta za vyumba 5 vya madarasa katika Shule ya Sekondari Kaigara;
- Kujenga vyoo vya walimu matundu 2 katika Shule ya Sekondari Itongo
- Ujenzi kuta wa vyoo matundu 3 katika Shule ya Sekondari Ruhanga

MCHANGO WA HALMASHAURI KWENYE MIRADI YA MAENDELEO

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi iliyotekelezwa kwa fedha za mapato ya ndani ni pamoja na Kuchangia mfuko wa wanawake na vijana, kununua na kusambaza vipando, kutengeneza na kusambaza madawati katika shule za msingi na sekondari, Kuchangia ujenzi na ukarabati wa miundombinu na majengo katika baadhi ya shule kama Shule ya Msingi Buyango, Shule ya Msingi Goziba, Shule ya Msingi Kairungu, Shule ya Msingi Mulambi, Shule ya Msingi Manyora, Shule ya Msingi Muyenje, Shule ya Msingi Rulanda, Shule ya

Msingi Kahengere na Shule ya Msingi Ngote. Hali hii imeongeza ufanisi na chachu ya maendeleo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio machache yaliyoelezwa hapo nyuma, bado kumekuwepo na changamoto kadhaa ambazo nyingine zimepatiwa ufumbuzi na nyingine zinaendelea kutafutiwa ufumbuzi, na hali hii imetufanya tuendelee kujitathmini na kujiandaa kufanya vizuri zaidi katika mwaka wa fedha huu tulio nao wa 2017/2018.

Kwa heshima kubwa na taadhima, ninapenda kuwashukuru Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za kudumu za Halmashauri, Waheshimiwa Madiwani wote na Wewe Mheshimiwa Mwenyekiti kwa msaada na utayari wa kushirikiana katika kupanga na kusimamia utekelezaji wa Mpango na Bajeti wa mwaka wa fedha 2016/2017. Aidha niwashukuru watendaji wote wa Halmashauri ya wilaya waliohusika katika idara zao ili kufanikisha utekelezaji mzuri wa majukumu ya Halmashari.

Kwa wote ninyi, naomba ushirikiano wenu pia katika mwaka huu wa fedha (2017/2018), ili tuendelee kuwa na mafanikio mema na kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi wetu.

Mungu awabariki, na asanteni kwa kunisikiliza.

Naomba kuwasilisha.

Emanuel Sherembi
Mkurugenzi Mtendaji (W)
Muleba